

ATHARI ZA SHERIA ZA MBEGU KWA MIFUMO YA MBEGU INAYOSIMAMIWA NA WAKULIMA



- 1 Mifumo ya mbegu inayosimamiwa na wakulima (FMSS) haitambuliwi na haiungwi mkono na sheria za mbegu, bali na jukumu muhimu inayotoa katika usambazaji na kudumisha aina mbalimbali ya mbegu na mimea.
- 1 Wakulima wadogo wanaosimamia mifumo yao ya mbegu hawashirikishwi katika mfumo rasmi wa mbegu wa nchi.
- 1 Wakulima wanaonekana kama watumiaji wa mbegu tu, na sio wadau muhimu katika mfumo wa mbegu.
- 1 Aina mbalimbali za mbegu za asili zinazozalishwa na wakulima wadogo hazitambuliwi na sheria za mbegu kwa sababu hazifikii kigezo cha DUS (ubainifu, kufafanana, na thabiti) na zinaonekana zisizo na ubora.
- 1 Wakulima wadogo hawawezi kumudu mbegu zilizothibitishwa kwa sababu ni ghali.
- 1 Baadhi ya sheria za mbegu huhalifisha uuzaji wa mbegu ambazo hazijathibitishwa. Hii huzuia uuzaji na ubadilishanaji wa mbegu kwa wakulima wadogo na ina athari hasi kwenye kipato chao.
- 1 Wakulima na asasi za kiraia wanapaswa kuendelea kutetea utambuzi na uungaji mkono wa mifumo ya mbegu inayosimamiwa na wakulima (FMSS).
- 1 Mifumo ya mbegu inayosimamiwa na wakulima inazingatia maswala muhimu kwenye uzalishaji wa mbegu – kama vile mahitaji ya lishe, mapendeleo ya ladha, umuhimu wa mila na desturi na uzalishaji wa aina mbalimbali ya vyakula – lakini sekta rasmi ya mbegu hupuuza mambo haya kwa sababu ya mtizamo wa kutengeneza faida.